**OFISI YA RAIS TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

**WIZARA YA ELIMU, SAYANSI, NA TEKNOLOJIA**

**HALMASHAURI YA WILAYA YA SERENGETI**

SHULE YA SEKONDARI IKORONGO,
S.L.P 100,
MUGUMU - SERENGETI.
TAREHE 18.12.2020.
SIMU: **0765157142, 0782537511.**

NDG,MZAZI / MLEZI WA ______________________________

YAH: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA MASOMO YA KIDATO CHA KWANZA KATIKA SHULE YA SEKONDARI IKORONGO MWAKA 2021.

**UTANGULIZI:**

Uongozi wa shule ya sekondari ya Ikorongo unayo furaha kukujulisha kwamba mwanao aliyekuwa akisoma shule ya msingi ______________________________ amechaguliwa kujiunga katika shule ya sekondari Ikorongo kidato cha kwanza mwaka 2021.

Shule ya sekondari ya Ikorongo ni shule ya **kutwa** yenye mchanganyiko wa **wavulana** na **wasichana.** Iko umbali wa km20 kutoka Mugumu mjini barabara iendayo Musoma upande wa kulia mwa barabara yapata mita 200 toka kibao cha shule. Shule iko MKOA wa Mara, WILAYA ya Serengeti, TARAFA ya Ikorongo, katika KATA mbili za Rung'abure na Kebanchabancha. Yapo mazingira mazuri ya mwanao kusoma na kuweza kufaulu ili kulisaidia Taifa, wazazi na yeye mwenyewe. Mwanao anatakiwa kuitumia vyema nafasi hii ya kusoma Ikorongo kama bahati kubwa kwani wapo wengi walioikosa nafasi hii muhimu.

Aidha, Mwanao anatakiwa kufika shule terehe **11/01/2021** bila kuchelewa tayari kwa kuanza masomo. Hata hivyo kuanzia tarehe **21.12.2020** wanafunzi wote waliochaguliwa kuja hapa shuleni wataanza maandalizi ya masomo "**Orientation course.**"

Ndimi

EMMANUEL M MIJA
MKUU WA SHULE.

MKUU WA SHULE
IKORONGO SEKONDARI
S.L.P. 100
MUGUMU-SERENGE

## 1. MAMBO YA KUZINGATIA

(A) Kila mwanafunzi atatakiwa aje shule na sare ya shule iliyoshonwa vizuri kwa maadili ya mwanafunzi awapo shule na nje ya shule.

- **Kwa wavulana**; Suruali mbili (02) za rangi nyeusi tetroni za kufungia kiunoni, zenye ruksi, ziwe pana, zenye mifuko miwili mbele na mmoja nyuma, ziwe na pindo miguuni chini, ziwe na marinda matatu (03) kwa mbele sehemu ya kunyooshea pasi, na ziwe zimeshonwa vizuri.
- **Kwa wasichana**; Sketi mbili (02) za rangi nyeusi nzito ndefu kuvuka magoti zenye marinda makubwa na ziwe na mfuko (mmoja).

(B) **KWA WOTE (Wavulana na Wasichana),** mahitaji ni haya yafuatayo:-

- Mashati meupe mawili (02) ya mikono mifupi
- Viatu vya ngozi jozi mbili (02) vya kawaida vyenye kamba
- T-shirt ya shule; rangi ya **PURPLE**, nzito na pana. Ni sare kwa wanafunzi wote kwa kidato cha kwanza.
- Soksi ndefu nyeupe jozi mbili (2)
- Nguo za michezo; Trucksuit, yaani suruali na jacket **rangi nyeusi.** Nzito, pana, raba za michezo za rangi nyeusi zenye kamba. Soksi ziwe za rangi yoyote.
- Cheti cha kuzaliwa original na copy kwa ajili ya usajili.
- Mfagio aina ya "***cherewa***" mmoja (01) kwa ajili ya usafi wa mazingira. Ni muhimu na lazima kwa wanafunzi wote.

**(C) VIFAA VYA DARASANI NA USAFI.**

- Daftari kubwa za (counter book 10), Mathematical set (bofa) lenye vifaa vya hisabati, rula ndefu, kalamu za wino za kutosha na penseli mbili , Kamusi ya kingereza (English Dictionary) moja (01)
- **Bunda moja (1) la karatasi yaani ream paper A4.** Kutakuwa na mazoezi mengi na mitihani
- **KITI NA MEZA Kuna upungufu mkubwa wa viti na meza hapa shuleni.**(Frem za chuma zenye raba).

**EMMANUEL M. MIJA**

**MKUU WA SHULE**

MKUU WA SHULE
IKORONGO SEKONDARI
S.L.P. 100
MUGUMU-SERENGE

## 2. SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE

A. Shule inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na inazingatia miongozo yote inayotolewa na wizara yenye dhamana ya Elimu nchini ambayo ni Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolijia. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yatafafanuliwa zaidi mara baada ya kuripoti shule.

- Heshima kwa viongozo, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima
- Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule ni muhimu
- Kuwahi katika kila shughuli za shule na nyingine utakazopewa
- Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo utakayopewa ya kuwa ndani ya mipaka ya shule kwa muda wote wa masomo utakapokuwa shuleni labda tu upewe ruhusa maalumu na kwa dharula tu.
- Kutunza usafi wa mwili wako na mazingira ya shule
- Kuvaa sare za shule wakati wote unapotakiwa uwapo shule
- Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote
- Michezo ni lazima kuhusika kwa kila ratiba ya michezo.

B. Makosa yafuatayo yanaweza kusababisha mwanafunzi kufukuzwa shule.

1. Wizi
2. Uasherati, ushoga na ubakaji
3. Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya kama cocaine, mirungi, kubeli n.k
4. Uvutaji bangi
5. Kupigana au kupiga
6. Kuharibu kwa makusudi mali ua Umma
7. Kudharau bendera ya taifa
8. Kuoa au kuolewa
9. Kupata mimba au kusababisha mimba ndani au nje ya shule.
10. Kutoa mimba
11. Kugoma, kuchochea, kuongoza au kuvuruga amani na usalama wa shule au watu
12. Kukataa au kugomea adhabu aliyopewa na Kiranja au Mwalimu kwa maksudi
13. Mwanafunzi kuwa na simu ya mkononi
14. Kutokuhudhuria vipindi bila ruhusa
15. Kutokufanya usafi maeneo ya shule
16. Kutokufanya majaribio au mitihani itolewayo na walimu.

**N.B.Tafadhali soma kwa makini maelekezo haya na kuyatekeleza kikamilifu.**

3. **Mambo menginemuhimu yanayo paswa kukamilishwa na kuwasilishwa shuleni na mwanafunzi.**
   - **a)** Fomu ya uchunguzi wa afya(Medical Examination Form) ambayo itajazwa na Mganga mkuu wa serikali.
   - **b)** Fomu ya maelekezobinafsi kuhusu historia ya mwanafunzi/ mkataba wa kutoshiriki katika migomo,fujo na makosa ya jinai.
   - **c)** Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria , kanuni na maelekezo mengine yatayotolewa na shule.

**KARIBU SANA IKORONGO SEKONDARI.**

Sahihi ya mkuu wa shule

EMMANUEL M.MIJA.
**MKUU WA SHULE.**

MKUU WA SHULE
IKORONGO SEK...ARI
S.L.P. 10...
MUGUMU-SERENGETI

**FOMU YA VIPIMO VYA MWILI NA AFYA YA MWANAFUNZI**

**FOMU HII IJAZWE NA MGANGA MKUU WA MKOA/WILAYA NA MWANAFUNZI AJE NAYO SHULENI SIKU YA KURIPOTI**

Mimi (Jina la Mganga Mkuu)..........................................................................

Ninathibitisha kuwa mwanafunzi huyu (Jina la Mwanafunzi) .....................................

Amepimwa kikamilifu na kuonekana kuwa anayo/hana afya nzuri kwa mujibu wa taarifa zifuatazo

A. HALI YA MWILI

I. Mapigo ya moyo..........................................................................
II. Haemoglobin ..............................................................................
III. Kundi la damu (blood group) ..........................................................
IV. Mkojo .....................................................................................
V. Kinyesi ....................................................................................
VI. Macho yana kasoro ........................................................................
VII. Masikio yana kasoro ......................................................................
VIII. Angalia; Weka maoni yako kuhusu kila kilichotajwa hapo juu baada ya vipimo
IX. MIMBA(Kwa wasichana).....................................................................

B. MAGONJWA

**Amewahi/ hajawahi / au hana magonjwa yafuatayo**

i. Bronchial Asthens .........................................................................
ii. Tuberculosis ..............................................................................
iii. Epilepsy .................................................................................
iv. Blood Pressure ............................................................................
v. Peptic ulcers...............................................................
vi. Sickle cells ..............................................................................
vii. Venereal Diseases (Give type) ...........................................................
viii. Mental Illiness (ugonjwa wa akili) ......................................................
**ix. Any other serious disease not mentioned above**

..............................................................................................

**Saini na muhuri wa Daktari**

**Tarehe.......................................**

**SHULE YA SEKONDARI IKORONGO**
**FOMU YA MAELEKEZO BINAFSI YA MWANAFUNZI PAMOJA NA AHADI YA UTII WA SHERIA ZA SHULE.**

1. Jina kamili ………………………………………………..
2. Anwani ya nyumbani……………………………………………………………………………………
3. Tarehe ya kuzaliwa …………………………………………………………………………………………
4. Mahali ulipo zaliwa , Kijiji/mtaa …………………………Kata……………….

   Tarafa ………………….. Wilaya …………………… Mkoa …………………..
5. Mahali unapoishi kwa sasa …………………………………………………………
6. Shule ya msingi ulikotoka …………………………………………………………..

   Anwani ………………………………………………………………………………
7. Dini l Dhehebu ……………………………………………………………………..
8. Watu wawili wa karibu ambao wanaweza kupelekewa taarifa zako za masuala ya shule.

……………………..                                        …………………………

Sahihi ya mwanafunzi.                                        Tarehe.

a) Mimi (Jina la mzazi/ mlezi wa mwanafunzi …………………………………………………

Mzazilmlezi wa ……………………………………………Nimesoma masharti na sheria za shule ya sekondari ya Ikorongo ambako mwanangu amechaguliwa kujiunga. Naahidi kuwa nitamuhimiza mwanangu kufuata sheria na taratibu zote za shule kama zilivyoelekezwa na kumtimizia mahitaji yake ya shule.

Aidha naahidi kushirikiana na uongozi wa shule katika malezi bora ya mwanangu ili kumwaandakuwa raia bora na mwema kwa Taifa letu.

……………………………………                                        ………………….

Sahihi ya mzazi/mlezi                                        Tarehe

MKUU WA SHULE
IKORONGO SEKONDARI
S.L.P. 100
MUGUMU-SERENGE